JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Tel No: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Morogoro Road,
S.L.P 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUANZA KWA VIKAO VYA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE.

Kamati Nne (4) za Kudumu za Bunge zitaanza Vikao Jumatatu, **tarehe 3 Agosti, 2026** katika **Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma**. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC). Kamati nyingine za Kudumu za Bunge zitaanza vikao Jumatatu**, tarehe 10 Agosti, 2026.**

Vikao hivi ni kwa ajili ya maandalizi ya **Mkutano wa Nne wa Bunge** unaotarajiwa kuanza siku ya **Jumanne, tarehe 25 Agosti, 2026.** Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati katika kipindi hicho ni:-

**a) Kupitia na Kuchambua Muswada wa Sheria**

(i) Kamati ya kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria itapitia na kuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa Mwaka 2026.

(ii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itapitia na kuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kilimo ya Mwaka, 2026 pamoja na Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka, 2026.

Miswada hiyo ilisomwa Mara ya Kwanza tarehe 26 Juni, 2026 wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge.



bungetz1 | bunge_tz | bunge.tanzania | Bunge TV | www.parliament.go.tz

**b) Kupitia na Kuchambua Sheria Ndogo**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo itapitia na kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge kwa mujibu wa **kifungu cha 10(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.**

**c) Kupokea na Kujadili Taarifa Mbalimbali za Utendaji wa Serikali na Taasisi zake**
Kamati Kumi na Moja (11) za Kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Serikali na Taasisi zake kwa mujibu wa **kifungu cha 7(1)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025**

Aidha, Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka Serikalini kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kusimamia, kuchambua, kuratibu na kulishauri Bunge kuhusu Sera za Fedha za Umma, Mapato ya Serikali, Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mujibu wa **kifungu cha 9 cha cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025**

**d) Kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
Kamati mbili zinazosimamia matumizi ya fedha za Umma zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu zilizokaguliwa za Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025. Kamati zinazohusika ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

**e) Kupokea na Kuchambua Taarifa ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itapokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

Ratiba ya shughuli za Kamati inapatikana katika tovuti ya Bunge ambayo ni ***www.bunge.go.tz***

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma
Ofisi ya Bunge
**Dodoma**

**01 Agosti, 2026**



bungetz1 | bunge_tz | bunge.tanzania | Bunge TV | www.parliament.go.tz